# Wanafunzi wanolewa madhara dawa za kulevya

**ARUSHA**

NA ZULFA **MFINANGA**

Ili kuhakikisha jamii inakuwa na vijana wenye maadili, serikali kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali ya Wilaya ya Meru mkoani Arusha imeanza kutoa elimu ya madhara ya dawa za kulevya kwa shule za msingi na sekondari.

Shirika la kijamii la Deploy and Nurturing Gallery (DNG - Tanzania) kwa kushirikiana na polisi Halmashauri ya Wilaya ya Meru wameanzisha kampeni ya kutoa elimu hiyo katika Shule ya Sekondari ya Maruvango kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne na kuwafikia wanafunzi 407.

Mratibu wa mafunzo hayo kutoka DNG Tanzania, Elizabeth Emmanuel, amesema kampeni imelenga kuwapatia ufahamu vijana hususan wanafunzi juu ya madhara ya dawa za kulevya kwa mtu mmoja mmoja, familia na taifa kwa ujumla.

"DNG Tanzania tumeona ni vema kushirikiana na Jeshi la Polisi hasa askari kata kutoa elimu hii kwa wanafunzi wetu ambao kimsingi ndio kizazi chetu cha kesho, kwani wakipata taarifa sahihi watafanya uamuzi sahihi kwa kuwa vijana wengi wanafanya uamuzi kupitia taarifa wanazopata," amesema Elizabeth.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Maruvango wakipata elimu ya madhara ya dawa za kulevya kutoka kwa Polisi-Kata, Inspekta Sai Nteminyanda.

Askari Kata ya Maruvango, Inspekta Sai Nteminyanda, ametoa elimu hiyo kwa kutumia picha kwa kuonyesha dawa halisi za kulevya ambazo ni mirungi, bangi, heroin, cocaine, gundi pamoja na kueleza madhara ya kila aina ya dawa.

Inspekta Nteminyanda amesema lengo la kutoa elimu hiyo kwa kutumia mifano halisi ya dawa hizo ni kusaidia wanafunzi hao kuzitambua kwa lengo la kuepuka kujihusisha nazo na kuwa mabalozi wazuri kwa vijana wenzao, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa juu ya watu wanaojihusisha na dawa hizo ili waweze kusaidiwa.

"Vijana wengi wanaingia katika matumizi ya dawa za kulevya kwa sababu mbalimbali ambazo kimsingi hazina mashiko ambazo ni pamoja na ushawishi, kisingizio cha maisha magumu, kutokuwa na elimu sahihi juu ya madhara yake, lakini kupitia nyie tunaamini elimu hii itasambaa sehemu kubwa na tutaokoa vijana wengi," amesema Inspekta Nteminyanda.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Maruvango, Henry Antto, ameomba kuanzishwa kwa klabu za kupinga dawa za kulevya shuleni hapo ili elimu hiyo iwe endelevu, kwa kuwa haipo katika mitaala ya elimu ambayo ni muhimu kwa mustakabali wa ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla.

Kampeni hiyo yenye kaulimbiu "Ukiona Dawa za Kulevya, Usithubutu, Usijaribu, Usionje" ni endelevu kwa vijana kote nchini, ambapo kwa sasa wanaendelea kutoa elimu kwa shule zote za msingi na sekondari Mkoa wa Arusha huku wakiomba wadau mbalimbali kujitokeza kusaidia katika kufanikisha lengo hilo.